KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 16, Issue 2
15th Dhul Hijjah 1432
11th Nov, 2011

YALIYOMO

AQEEDA ... 1 - 4

'EID MBILI NA HUKMU... 4

SHERH 'AQEEDAT AT-TAHAAWIYYAH AL-MUYASSAR

Dr: Muhammad bin Abdur-Rahman al-Khumayyis

Kila Sifa njema ni zenye kumthubutukia Mwenyezi Mungu, Tunamsifu Yeye, na tunatarajia msaada Wake na msamaha kutoka Kwake. Tunajilinda kwa Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wata'aalah) kutokana na maovu ya nafsi zetu na kutokana na udhaifu wa vitendo vyetu. Yeyote alieongozwa na Mwenyezi Mungu, hakuna yeyote awezae kumpotoa, na Yeyote aliepotolewa na Mwenyezi Mungu, hakuna yeyote awezae kumuongoza. Nashuhudia yakwamba hapana mungu wa kweli anaestahiki kuabudiwa isipokuwa Allah, Peke Yake, pasi na mwenzi wala mshirika. Nazidi kushuhudia yakwamba Muhammad ni Mtumwa wake wa kweli na Mtume. Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wata'aalah), Azifikilize Amani na Baraka Zake juu ya Mtume wa mwisho Muhammad, juu ya ahli zake wema na waliotahirika, na juu ya maswahaba zake wote watukufu.

Enyi watu! Mcheni Mola wenu (Allah) ambaye amekuumbeni katika nafsi (asli - Aadam) moja. Na akamuumba mkewe katika nafsi ile ile. Na akaeneza wanaume wengi na wanawake kutoka katika wawili hao. Na mcheni Mwenyezi Mungu ambaye kwaye mnaombana. Na (mwatazame) jamaa. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mlinzi juu yenu (Anayaona kila mnayoyafanya). [Soorah an-Nisaa 4:1]

Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu (kwa kuyatekeleza yote ambayo Aliyowaamrisha na kujiepusha na yote ambayo Aliyowakataza) kama ipasavyo kumcha; wala msife isipokuwa mmekwishakuwa Waislamu kamili. [Soorah Aali Imraan 3:102]

Enyi mlioamini! Muogopeni Mwenyezi Mungu na semeni maneno ya haki. Atakutengenezeeni vizuri vitendo vyenu na Atakusameheni madhambi yenu; Na anayemtii Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, bila shaka amefanikiwa mafanikio makubwa. [Soorah al-Ahzaab 33:70-71]

Ammaa Ba'ad:

Kwa hakika maneno yalio ya kweli kabisa ni yale ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu (Qur'aan) na uongofu ulio bora zaidi ni ule wa Muhammad (Sallallahu 'alayhi wasallam). Na maovu yalio mabaya zaidi ni mambo ya kuzua (yalio mageni katika mafundisho ya Uislamu), na kila jambo lilozuliwa (katika Dini) ni Bid'ah, na kila Bid'ah ni Dhalaalah (njia mbaya, upotofu), na kila Dhalaalah mwisho wake ni motoni.

Kisha Amma ba'd: Kwa hakika huu ni ufafanuzi kwa mukhtasar kuhusu ubainifu wa 'aqeedah ya Ahlus-Sunnah wal-Jamaa'ah kulingana na madh-hab ya Wanazuoni wa Ki-Islamu: Abee Haneefah An-Nu'maan bin Thaabit al-Koofee, na Abee Yoosuf Ya'qoob bin Ibraahim al-Ansaari, na Abee 'Abdullaah Muhammad bin al-Hassan ash-Shaybaani. 'Aqeedah hii ambayo iliyopokewa na kunukuliwa kutoka kwao na al-Imaam Abu Ja'far at-Tahaawi. Hapana shaka yakwamba Imaam at-Tahaawi, Mwenyezi Mungu Awe Radhi nae, aliitekeleza kazi hii kwa uhodari maridhia na kuleta manufaa makubwa. Na ni kwanini isiwe hivyo, haliyakuwa yeye alisifika kwa uaminifu wake katika kuyathibitisha yale aliyoyapokea kutoka kwenye vitabu vya 'aqeedah vya Wanavyuoni hao wakubwa waliotajwa, kwa kutumia misingi aliyokuwa nayo imara ya ki-elimu na ujuzi wake kuhusiana na madh-hab ya ki-Hanafee. Nae alikuwa ni mbora wa wapokezi wa 'aqeedah za hawa ma-Imaam, kwani alikuwa ni muaminifu wa kutegemewa miongoni mwa wanavyuoni wa fiqh na hadeeth. Maandishi hayo yaliyopokewa na Imaam at-Tahaawi yakachukuliwa kwa muafaka wa Umma mzima. Mafafanuzi na maelezo ya waliokuja baadae yakakithiri, wakapatikana miongoni mwao wale walioafikiana na sunnah na wengineo wakaandama njia za wataalamu wa elimu ya filosofiya (***philosopher***) Sherhe ya al-Imaam Ibn Abee al-'Izz al-Adhra'ee al-Hanafee (rahimahullaah) ndiyo iliyokuwa bora na yenye kufaidisha mno miongoni mwa sherhe zote. Katika uchambuzi wake, aliyapambanua na kuyachungua masala ya Imaam at-Tahaawi katika 'aqeedah hii kwenye mafungu matatu:

<u>LA KWANZA:</u>

Maneno yake Imaam at-Tahaawi: (***Qadeemun bilaa ibtidaa' – Utangu wake usokuwa na mwanzo***): Haya ni miongoni mwa mambo ya kuzua ya watu wa elimu ya philosophia. Wala Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wata'aalah) na asiitwe majina isipokuwa kwa yale Aliyojiita nayo Yeye mwenyewe, au Aliyomuita kwa majina hayo Mtume wake (Sallallaahu 'alayhi wasallam).

<u>La pili:</u>

Maneno yake: (***Ta'aala 'anil hudood wal ghaayaat wal arkaan wal a'dhaa' wal adawaat* – Yeye yuko juu ya mipaka yake, na juu ya upeo, na juu ya miimo (nguzo), na juu ya viungo vya mwili na vitenda kazi**): Na maneno haya hakuna katika misingi ya dini (Shar'), si kwa njia ya ukanushaji wala njia ya kuthibitisha, lakini haya ni mambo ya uzushi ya wataalamu wa filosofia. Ni aula kujishikamanisha na maneno yenye misingi ya dini (Shar').

<u>La tatu:</u>

Katika kuyakariri maneno: (***Annal Eemaan iqraar bil lisaan watasdeeq bil janaan*** - **Yakwamba Eemaan ni kutamka kwa ulimi na kusadikisha kwa nyoyo**): Kwa matamshi hayo, akaondosha au akafutilia mbali vitendo vyote vijulikanavyo kwa majina

(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

ya imaan. Na huku ni kwenda kinyume na kongamano la jamhuri ya Salaf kutoka katika madh-hab tafauti. Mwenyezi Mungu Awarehemu ma-Imaam wawili: at-Tahaawi na Ibn Abee al-'Izz, na ma-Imaam wote waliobaki kwa ujumla kwa utumishi wao katika Sunnah na 'aqeedah ya Ahlus-Sunnah wal-Jamaa'ah.

Nikapendelea mimi kuisherehe (kuichambua) 'aqeedah hii kwa mukhtasar kwa ajili ya wanafunzi wapya miongoni mwa wanaotafuta ilimu ili wawafaidisha watu wengine.

Ninamuomba Mwenyezi Mungu Akija'alie kitabu hichi kiwe na manufaa kwa Waislamu na Anizidishie uzito katika mizani yangu.

Mwenyezi Mungu Yuko nyuma ya makusudiwa yangu na Yeye Ananitosheleza, Nae ni Mlinzi bora kabisa. Na ulinganizi wetu wa mwisho ni kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu wote.

MLANGO WA KWANZA:

AMESEMA AL-IMAAM AL-HUJJAH ABU JA'FAR AL-WARRAAQ AT-TAHAAWI KUTOKA MISR (RAHIMAHULLAAH)

Haya ni makumbusho ya ubainifu wa 'aqeedah ya Ahlus-Sunnah wal-Jamaa'ah kulingana na madh-hab ya Wanazuoni wa Ki-Islamu: Abee Haneefah An-Nu'maan bin Thaabit al-Koofee, na Abee Yoosuf Ya'qoob bin Ibraahim al-Ansaari, na Abee 'Abdullaah Muhammad bin al-Hassan ash-Shaybaani, radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao wote. Na yale wanayoamini kuwa ni miongoni mwa misingi ya dini na wakayatenda kwa mnasaba wa dini kutoka kwa Mola wao.

[1] Katika Tawheed, tunapompwekesha Mwenyezi Mungu, huwa tunaitakidi yakwamba uwezo wote, yaani "taufeeq" unatokamana na Mwenyezi Mungu:

[1] Hakika Mwenyezi Mungu ni mmoja wala hana mshirika:

Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu ni mpweke katika kila kitu, katika dhati yake, katika vitendo vyake, katika majina Yake na sifa Zake, na katika kustahiki kuabudiwa kwake. Hana mshirika katika yote hayo. Na wala hana mshirika katika kuumba kwake na Amri Zake.

Amesema Mwenyezi Mungu (*Subhaanahu wata'aalah*):

Fahamuni, Kuumba (ni Kwake tu Mwenyezi Mungu) na amri zote ni Zake (Mwenyezi Mungu). - [Soorat al-A'raaf 7:54]

na akasema:

Je, yuko muumba mwengine asiyekuwa Mwenyezi Mungu, anayekupeni riziki kutoka mbinguni au ardhini? – [Soorat Faatir 35:3]

.Wala hana mshirika katika kuleta manufa'a, madhara, kufisha, kuhuisha na mengine yasiyokuwa hayo kuhusiana na mas-ala ya Uwezo wa kufanya Atakavyo katika Ulimwengu huu.

Na vilevile hana mshirika katika majina yake wala katika sifa zake, na wala hana mshirika katika Uola wake (**ULOOHIYYAH)** na katika kustahiki kuabudiwa kwake. Na wala tawheed ya mja haitimii mpaka ajitakase na aina zote hizi za shirk. Na atekeleze mambo yanayokwenda kinyume cha hayo katika aina mbalimbali za tawheed zinazompasa. Inampasa ampwekeshe Mwenyezi Mungu katika Uola wake na vitendo vyake, ampwekeshe katika majina yake na sifa zake. Wala asiwape viumbe sifa zinazopasa kusifiwa nazo Muumba. Na ampwekeshe katika uola wake bila ya kunyenyekea katika ibada kisichokuwa Mwenyezi Mungu.

Akasema Mwenyezi Mungu (*Subhaanahu wata'aalah*):

Wewe tu ndiye tunayekuabudu, na Wewe tu ndiye tunayekuomba msaada. - [Soorat al-Faatihah 1:5]

Na pia akasema:

Sikuwaumba majini na watu ila wapate kuniabudu. - [Soorat adh-Dhaariyaat 51:56]

[2] Wala hapana chochote mfano wake:

Hii ndiyo asili ya Tawheed, yaani kuitakidi yakwamba Mwenyezi Mungu (*Subhaanahu wata'aalah*)

Hakuna chochote mfano wake; naye ni Mwenye kusikiya, Mwenye kuona. [Soorat ash-Shoorah 42:11]

Mwenyezi Mungu Hafanani na yeyote miongoni mwa viumbe vyake, si katika Dhati Yake, wala katika Vitendo vyake, wala katika Majina Yake, wala katika Sifa Zake na wala si katika Haki Zake.

[3] Hapana chenye kumshinda:

Kwa maana yakwamba Yeye Mwenyezi Mungu Aliye Mtukufu ni Muweza wa kufanya Atakavyo.

Hakika amri yake anapotaka chochote (kile kitokee) ni kukiambia: 'Kuwa,' basi mara huwa. [Soorat Ya-Sin 36:82].

Hakuna kitu chochote kigumu wala chenye kumshinda,

Na hakuna kitu kinachoweza kumshinda Mwenyezi Mungu mbinguni wala katika ardhi. Bila shaka yeye ni Mwenye kujua, Mwenye uweza. [Soorat Faatir 35:44].

Yote hayo ni katika kutimia kwa uwezo Wake na Ukamilifu wake *(Subhaanahu wata'aalah)*.

Anayopenda Mwenyezi Mungu yanakuwa na asiyoyapenda Mwenyezi Mungu hayawi. Msemo huu unathibitisha ukamilifu wa **UOLA** wake (*Subhaanahu wata'aalah*) **(RUBOOBIYYAH)**.

[4] Wala hapana Mola asiyekuwa Yeye:

Haya ni matamshi ya Tawheed, nayo yalitamkwa na Mitume wote waliopewa ujumbe.

Na bila shaka tulimpeleka Mtume katika kila uma yakwamba "Muabuduni Mwenyezi Mungu na mwepukeni (Iblisi) muovu." [Soorat an-Nahl 16:36]

Na maana yake: Hapana anaestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah Peke Yake, kwa sababu Yeye ndiye Muumba Anayewaruzuku waja wake, na Mfalme Mwenye kuwapangia waja malimwengu yao. Kwahivyo, hakuna chengine chochote kinachostahiki kuabudiwa kinyume na Yeye katika kila aina ya ibada. Na yoyote au chochote kinachoabudiwa kinyume cha Mwenyezi Mungu, basi hiyo ni ibada isiyofaa.

Hayo ni kwa sababu Mwenyezi Mungu yuko; na wale wanaowaabudu badala yake (Mwenyezi Mungu) hao ni batili. [Soorat al-Hajj 22:62]

Na hayo ni kwa sababu wao (viumbe) hawamiliki kitu chochote katika maamrisho, wala usimamizi, wala mambo yanayohusiana na mipango ya watu ya ki-maisha. Ukiyachunguza na kuyatafakari maneno hayo, utakuta yakwamba ndani yake muna makatazo ya kufanya ibada kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu, kisha ikathibitishwa ibada ya kuabudiwa Yeye peke yake. Vilevile kunapatikana ndani yake ukafiri kwa yule anaemuabudu asiyekuwa Mwenyezi Mungu, kisha ikathibitishwa ibada yenye kumkusudia Yeye peke yake. Na hiyo ndiyo **Tawheed al-Uloohiyyah**.

Kwa Mukhtasar:

Hakika Mwenyezi Mungu *(Subhaanahu wata'aalah)* ni mmoja katika dhati Yake, na majina Yake, na sifa Zake, na ni mmoja katika kustahiki kuabudiwa kwake. Wala hakuna kitu chochote kinachofanana na Yeye katika viumbe vyake kwa sifa yoyote, na Yeye ni muweza wa kila kitu.

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 3)

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

Hakuna kitu chochote chenye kumshinda na wala hakuna kitu chochote kigumu kwake Yeye, kama ambavyo hakuna anaestahiki kufanyiwa ibada isipokuwa Yeye Peke yake *(Subhaanahu wata'aalah).*

Masuali:

1. Ni nini maana ya kumpwekesha Mwenyezi Mungu *(Subhaanahu wata'aalah)*?
2. Ni zipi aina tatu za Tawheed?
3. Ni zipi aina tatu za Shirk?

Taja maneno ambayo yaliyolinganiwa na Mitume wote.

MLANGO WA PILI:

[5] Ni wa tangu kusokuwa na mwanzo na ni wa kudumu kusokuwa na mwisho:

Al-Qadeem - القديم: Hili si jina la Mwenyezi Mungu *(Subhaanahu wata'aalah).* Kinachokusudiwa hapa ni kwamba Utukufu ni wa Mwenyezi Mungu *(Subhaanahu wata'aalah)* ambae hapana kilichomtangulia kama vile ambavyo Yeye ni wa kudumu milele kusokuwa na mwisho. Na hiyo ndiyo maana ya Maneno Yake *(Subhaanahu wata'aalah):*

Yeye ndiye wa mwanzo na ndiye wa mwisho. [Soorat Al-Hadyd 53:3]

Kwahivyo Yeye ni wa mwanzo na hakuna chochote kilichokuwa kabla yake, na ni wa mwisho na hakuna chochote baada yake. Na akatufafanulia maana ya aya hiyo Mtume wa Mwenyezi Mungu *(Sallalllaahu 'alayhi wasallam)*.

[6] Hatoweki wala haangamii:

Kama alivyosema Mwenyezi Mungu *(Subhaanahu wata'aalah)*:

Kila kilichoko juu yake (ardhi na mbingu) kitatoweka, (kitaondoka). Utabaki Uso wa Mola wako (tu Mwenyewe) Mwenye Utukufu na Heshima. [Soorah Ar-Rahmaan 55:26-27]

Na pia kama alivyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

Kila kitu kitakufa isipokuwa Yeye (Mwenyezi Mungu) [Soorat Al-Qasas 28:88]

Kwahivyo Mwenyezi Mungu *(Subhaanahu wata'aalah)* huwafisha viumbe vyake na wala Yeye hafi, huviondoa viumbe vyake na wala Yeye haondoki, bali Yeye *(Subhaanahu wata'aalah)* atabakia milele baada ya kila kitu.

[7] Hakuna kinachokuwa ila apendavyo:

Kwa hakika Mwenyezi Mungu *(Subhaanahu wata'aalah)* ni muweza wa kila kitu. Akasema *(Subhaanahu wata'aalah)*:

Lakini Mwenyezi Mungu hufanya anayoyataka. [Soorat Al-Baqarah 2:253]

Pindi Mwenyezi Mungu akipenda jambo lolote litokee, utalikuta ni lenye kutokea hata kama ni kinyume cha mapendelewa ya viumbe vyake. Na kama akipenda jambo lisitokee, basi viumbe vyake wote kwa umoja wao hawawezi kulifanya. Kwahivyo, hii ndiyo rada ya maamrisho yenye makadirio ya Mwenyezi Mungu yajulikanayo kama:

(*al-iraadat al-kawniyyatu al-Qadariyyah*) الإرادة الكونية القدرية

Ambayo yasokuwa na badala. Kwa hakika kila jambo la kheri na la shari linalotokea katika matukio haya limekuja kutokana na mapendelewa na khiyari Yake (*Subhaanahu wata'aalah*). Wala hakuna kitu chochote kiwezacho kuishinda khiyari ya Mwenyezi Mungu. Kila apendacho Mwenyezi Mungu (kiwe) huwa, na kila asichopenda kisiwe, hakiwi. Na dalili ya maneno haya ni nyingi mno.

[8] Hakuna dhana iwezayo kumuwaza, na wala hakuna fahamu imfikiayo:

Kwa hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu hakumuwezesha yoyote miongoni mwa waja wake (amjue Yeye vilivyo) katika ilimu yake, kama alivyosema (*Subhaanahu wata'aalah*):

(Mwenyezi Mungu) Anajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao. Wala wao hawawezi kumjua (Mungu) vilivyo. [Soorat Taa-ha 20:110].

Hakuna dhana iwezayo kumuwaza, na wala hakuna fahamu imfikiayo wala kuwa na mfano wake (katika akili yako) na hata kujaribu kuwa na fikra ya Umbile lake, na wala hakuna yoyote miongoni mwa viumbe vyake amjuae Mwenyezi Mungu katika dhati yake.

[9] Na wala hafanani na kiumbe chochote:

Kama ilivyo yakwamba Yeye hafanani na yoyote miongoni mwa viumbe vyake katika dhati yake wala katika majina yake, vilevile Mwenyezi Mungu (*Subhaanahu wata'aalah*) hafanani na viumbe vyake katika sifa zake wala katika vitendo vyake. Kutakasika ni kwake na Aliyetukuka, hakuna chochote mfano wake.

[10] Mwenye uhai wa maisha ambae asokufa, msimamizi wa kila jambo asiyelala:

Kutakasika ni kwake (Mwenyezi Mungu) aliye Juu yu hai wala hafi, kama alivyosema (*Subhaanahu wata'aalah*):

Na umtegemee (Mwenyezi Mungu) wa milele Ambaye hatakufa. [Soorah al-Furqaan 25:58]

Na Akasema:

Kila kilichoko juu yake (ardhi na mbingu) kitatoweka, (kitaondoka). Utabaki Uso wa Mola wako, Mwenye utukufu na heshima [Soorah ar-Rahman 55:26-27]

Na Akasema:

Kila kitu kitakufa isipokuwa Yeye (Mwenyezi Mungu Peke Yake) [Soorat al-Qasas 28:88]

Kwahivyo Mwenyezi Mungu (*Subhaanahu wata'aalah*) yu hai wala hafikwi na mauti, nae ni msimamizi wa kila jambo, kusinzia hakumshiki wala kulala. Isipokuwa Amejitenga ulimwengu mzima uzani vipimo, bali Yeye ndiye msimamizi wa kila jambo juu ya maamrisho ya ufalme wake (*Subhaanahu wata'aalah*).

Kwa haya yote yaliyotangulia kutajwa, wamekosolewa *al-mushabbihah* ambao wameshabihisha Mwenyezi Mungu (*Subhaanahu wata'aalah*) na viumbe vyake, na kwa ajili hiyo wakakufuru.

[11] Anaumba pasi na kuwa na haja, Anaruzuku pasi na kuona taklifu:

Hakika Mwenyezi Mungu (*Subhaanahu wata'aalah*) hakuwaumba viumbe kwa kuwa na mahitaji yoyote kutoka kwao au kuwa na tamaa ya jambo lolote au msaada wowote, bali aliwaumba ili wamuabudu. Akasema Mwenyezi Mungu (*Subhaanahu wata'aalah*):

Sikuwaumba majini na watu ila wapate kuniabudu. [Soorat adh-Dhaariyaat 51:56]

Na Yeye (*Subhaanahu wata'aalah*) ndiye mwenye kuwaruzuku viumbe vyake wote wakiwemo watu na majini, ndege na wanyama mwitu, na wengine wasokuwa wao, aliye na imani (*Mu'min*) na kafiri. Na humpa kila mmoja miongoni mwao kila wanachomuomba bila ya kupungua chochote kutoka katika ufalme wake. Anazo funguo za mbingu na ardhi Mikononi mwake.

[12] Hufisha bila ya kuwa na khofu na hutia uhai bila ya tabu:

Na Yeye (*Subhaanahu wata'aalah*) huwaondolea maisha (huwafisha) viumbe vyake bila ya kuwa na khofu yoyote.

Mwenyezi Mungu hutakabadhi roho wakati wa mauti yao. [Soorat az-Zumar 39:42]

Na hakuna wa kupinga hukumu yake. Naye ni mwepesi wa kuhisabu. [Soorat ar-Ra'd 13:41]

Akasema Mwenyezi Mungu (*Subhaanahu wata'aalah*):

Haulizwi (Mwenyezi Mungu) anayoyafanya (kwani yote ni ya haki)

(Endelea kutoka Uk. 3)

lakini wao (viumbe) wataulizwa. [Soorat al-Anbiyaa' 21:23]
Na Yeye ndiye atakaewafufua waliokufa siku ya kiyama.
Waliokufuru wanadai kuwa hawatafufuliwa. Sema: "Kwa nini? Kwa haki ya Mola wangu nyinyi lazima mtafufuliwa; kisha lazima mtajulishwa mliyoyatenda (na mlipwe kwayo). Na hayo ni sahali kwa Mwenyezi Mungu." [Soorat at-Taghaabun 64: 7]
"Mola wetu! Wewe ndiwe Mkusanyaji wa watu katika Siku isiyo na shaka ndani yake…" [Soorat aali-Imraan 3:9]
Kwa hakika Mwenyezi Mungu (*Subhaanahu wata'aalah*) atawafufua watu baada ya kufa kwao siku ya kiyama. Na hilo ni jambo lisilo na shaka. Kwahivyo yule ambae anaye huisha ardhi baada ya kufa kwake kwa maji ambayo huotesha mimea ni muweza wa kuwahuisha waliokufa:
Basi namna hivi tutawafufua wafu, ili mpate kukumbuka. [Soorat al-A'raaf 7:57]
Na yule ambae aliyewaumba mara ya kwanza ni muweza wa kuwarejesha kwa mara nyengine (baada ya kufa kwao), na hilo ni jepesi kwake. Ameepukana (Mwenyezi Mungu) na upungufu, na Yu juu kuliko yale wanayomsifu nayo.

Kwa Mukhtasar:

Kwa hakika Mwenyezi Mungu (*Subhaanahu wata'aalah*) ni wa mwanzo na ni wa mwisho, wa milele ambae hatakufa, anaefanya apendavyo na hapana ajuae (yaliyo katika) ilimu yake. Kusinzia hakumshiki wala kulala, haulizwi (Mwenyezi Mungu) anayoyafanya (kwani yote ni ya haki) lakini wao (viumbe) wataulizwa.

Masuali:

Jee, (***al-Qadeem*** - (**القديم**ni miongoni mwa majina ya Mwenyezi Mungu?
Ni nini maana ya "Hakuna kinachokuwa ila apendavyo".
Jee Shirk inayofanywa na watu ni kwa ajili ya mapendelewa ya Mwenyezi Mungu?

(Endelea kutoka Vol 16, Issue 1)

'EID MBILI NA HUKMU ZAKE

Katika riwaya ya al-Bukhari, amesema 'Aishah: "Mtume (صلى الله عليه وسلم), aliingia nyumbani na mimi nilikuwa na wasichana wawili waliokuwa wakiimba nyimbo za vita vya Bu'ath. Mtume (صلى الله عليه وسلم) akalala kitandani na akageuza uso wake upande mwengine. Abu Bakr akaingia na akaanza kunikaripia, zana za miziki za Sheitwaan mbele ya Mtume (صلى الله عليه وسلم)!' Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamkabili na kumwambia: 'Wachana nao' Abu Bakr aliposita, nikawakonyeza wale wasichana na kuafunzia waondoke. Ilikuwa ni siku ya 'Eid na Waafrika walikuwa wakicheza na ngao zao pamoja na mikuki yao. Emma mimi nilimuuliza au Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliniuliza iwapo nilipendelea kuendelea kuwatazama [sasa hivi sikumbuki vizuri]. Nami nikakubali. Kutokana na ruhusa hii, ndipo niliposimama nyuma yake na mashavu yangu yakawa yamegusana na mashavu yake. Akawa ananiambia: 'Endelea, ewe kabila la Arfadah, mpaka nikachoka: kisha Mtume (صلى الله عليه وسلم) akaniuliza: 'Umetosheka?' Nikamjibu, "Na'am.": "Haya nenda zako sasa." " [***Swaheeh Al-Bukhari***: vol.2, Uk. 37, no. 70 . ***Swaheeh Muslim***: vol. 2, Uk. 420-1, no. 1942].
Ibn Hajar amenukuu katika Fath al-Baaree, "Amesimulia Ibn as-Siraj kutoka kwa Abu az-Zinad, nae kutoka kwa 'Urwah kutoka kwa 'Aishah yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema siku hiyo: 'Mayahudi wa Madeenah na wajue yakwamba Dini yetu ni kundufu [na kwamba ina nafasi ya mapumziko] na mimi nimeletwa na Dini nyepesi isiyokuwa na mirengo."'
Muslim amepokea kutoka kwa Nubaishah yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "Masiku ya Tashreeq [siku ambazo 'Eid inasherehekewa] ni masiku ya kula na kunywa [isiyokuwa vyenye kulevya] na kumkumbuka Allaah (سبحانه وتعالى)."

9. UBORA WA 'AMALI NJEMA KATIKA SIKU ZA MWANZO ZA DHUL-HIJJAH.

Amepokea Ibn 'Abbas yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: ***"Hapana 'amali njema zinazofanywa katika masiku mengine zitakazokuwa na malipo makubwa kuliko zile zenye kufanywa katika masiku haya [maana yake masiku kumi ya dhul-Hijjah]."***
Maswahaba wakauliza: "Yaa Rasoolullaah, hata pia Jihaad katika njia ya Allaah?" Akawajibu: "Hata pia Jihaad isipokuwa kwa yule aliyeweka maisha yake na mali yake katika hatari [kwa ajili ya Allaah] na asirudi na chochote katika hayo."
Ahmad na At-Tabaraanee wamepokea kutoka kwa Ibn 'Umar yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "Hakuna siku iliyo na heshima kubwa mbele ya Allaah na hakuna vitendo vyenye kupendekeza mbele ya Allaah kuliko masiku zile zilizomo ndani ya masiku kumi haya. Kwahiyo semeni tahleel [Hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah], takbeer [Allaahu Akbar] na tahmeed [kila sifa njema ni za Allaah] kwa wingi [katika masiku hayo]."
[***Irwaa ul Ghaleel***: vol. 3, Uk. 398-9.]

10. Tahadhari dhidi ya kutenda maovu:

1. Baadhi ya watu hudhania kuwa Uislamu umetuambia tukeshe na kuswali katika usiku wa 'Eid, wakishikilia hoja hadeeth ambayo si swaheeh isemayo yakwamba, 'Yoyote mwenye kukesha na kuswali katika usiku wa 'Eid, basi moyo wake hautokufa siku ambayo nyoyo zitakapokufa." Hadeeth hii imepokewa kwa isnaad mbili, na mojawapo ni dha'eef, na hiyo nyengine ni dha'eef mno.[Angalia katika ***Al-Fawaaidul Majmoo'ah***: cha Imaam Ash-Shaukaanee: Uk. 71]. Uislamu haujatwambia kuupwekesha usiku wa 'Eid kwa kukesha na kuswali; lakini iwapo mtu ni mzoefu wa kukesha na kuswali usiku (qiyaam), basi hapana matatizo na mtu huyo kukesha na kuswali katika usiku wa 'Eid.
2. Mchanganyiko wa wake na waume kwenye baadhi ya sehemu za kuswali, mabarabarani na kadhaalika; ni mambo ya kusikitisha yakwamba haya hufanyika tena sio kwenye misikti ya kawaida tu, bali hata kwenye sehemu zilizobarikiwa miongoni mwazo, al-Masjid ul Haraam [iliyoko Makka]. Wanawake wengi—Twamuomba Allaah awaongoze—hutoka bila ya kujisitiri, wakiwa wamejipamba, wakajitia manukato, na kujirembesha haliyakuwa kuna mkusanyiko mkubwa kama huo msikitini—hatari za hali kama hizi ziko wazi. Kwahiyo wale wenye mamlaka ni lazima wapange swala za 'Eid kisawasawa, kwa kuweka milango na njia maalum kwa wanawake na kuchelewesha kuondoka kwa wanaume mpaka pale wanawake watakapokuwa wameondoka.
3. Baadhi ya watu hukusanyika pamoja katika siku ya 'Eid kwa min-ajil ya kuimba na mambo mengine ya upuzi na starehe, na jambo hili haliruhusiwi.
4. Baadhi ya watu husherehekea 'Eid kwa sababu Ramadhaan huwa imekwisha na hawatakuwa na haja ya kufunga tena . Haya ni makosa, waumini husherehekea 'Eid kwa sababu Allaah amewasaidia kuukamilisha mwezi wa kufunga, sio kwa sababu kule kufunga, ambako watu wengine huchukulia kuwa mzigo mzito ndio umemalizika.